**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# TAAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA WAFANYABIASHARA/WAKULIMA WENYE NIA YA USAFIRISHAJI WA PARACHICHI NA NDIZI MBICHI KWENDA JAMHURI YA AFRIKA YA KUSINI

**Arusha, 24 Septemba, 2026**

Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), kwa Mamlaka iliyonayo kama Shirika la Kitaifa la Ulinzi wa Mimea (National Plant Protection Organization – NPPO) la Tanzania, inawatangazia Wafanyabiashara, Wakulima, Wazalishaji na Wasafirishaji wenye nia ya kusafirisha parachichi na ndizi mbichi kwenda Jamhuri ya Afrika ya Kusini kuwasilisha maombi kwa ajili ya kushiriki katika taratibu za uhakiki wa uzingatiaji wa mahitaji ya afya ya mimea ya nchi hiyo.

Mchakato huu unalenga kuthibitisha kuwa mahali pa uzalishaji (places of production), vituo vya kufungashia (packing facilities), mifumo ya uzalishaji na utunzaji wa bidhaa zinazopelekwa nje zinazingatia hatua zinazohitajika za Afya ya Mimea (phytosanitary measures) kwa mujibu wa mahitaji ya nchi inayoagiza na viwango husika vya kimataifa vya Afya ya Mimea.

## 1. MUDA WA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yatapokelewa na TPHPA kuanzia: **24 Septemba, 2026 – 06 Oktoba, 2026. Waombaji** wanapaswa kuwasilisha maombi yao mapema ili kuwezesha TPHPA kufanya uhakiki wa nyaraka na kupanga ukaguzi wa afya ya mimea na uhakiki wa uzingatiaji wa mahitaji (phytosanitary inspection/compliance audit) kwa wakati.

## 2. NYARAKA NA TAARIFA ZINAZOTAKIWA

Waombaji wanatakiwa kuwasilisha barua rasmi ya maombi pamoja na nyaraka na taarifa husika za kila zao, zikiwemo:-

i. Cheti cha usajili wa kampuni;
ii. Cheti cha TIN;
iii. Leseni ya biashara;
iv. Taarifa za mahali pa uzalishaji (place of production), ikiwemo eneo, ukubwa na taarifa za uzalishaji;
v. Taarifa za kituo cha kufungashia (packing facility) kinachohusika;
vi. Mfumo wa ufuatiliaji wa bidhaa (traceability) kuanzia mahali pa uzalishaji hadi kusafirishwa;
vii. Taarifa za usidhibiti wa visumbufu (wadudu na magonjwa) vya mimea katika mahali pa uzalishaji;
viii. Kumbukumbu za ufuatiliaji na udhibiti wa visumbufu (wadudu na magonjwa) vya mimea;
ix. Taarifa za matumizi ya viuatilifu, pale inapohitajika;
x. Nyaraka au taarifa nyingine zitakazohitajika na TPHPA kwa ajili ya kuthibitisha uzingatiaji wa mahitaji ya afya ya mimea ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini.

## 3. UKAGUZI WA AFYA YA MIMEA

Baada ya kupokea na kuhakiki maombi na nyaraka husika, TPHPA itafanya ukaguzi wa afya ya mimea (phytosanitary inspection) pamoja na uhakiki wa uzingatiaji wa mahitaji husika katika maeneo ya uzalishaji na vituo vya kufungashia, kwa waombaji watakaokidhi vigezo. Ukaguzi huo unatarajiwa kufanyika Kuanzia tarehe **07 Oktoba 2026.**

## 4. UWASILISHAJI WA TAARIFA KWA NPPO YA AFRIKA YA KUSINI

Baada ya kukamilika kwa ukaguzi na kuthibitishwa kwa uzingatiaji wa mahitaji husika, TPHPA itawasilisha taarifa za waombaji wanaokidhi mahitaji kwa Shirika la Kitaifa la Ulinzi wa Mimea (NPPO) la Jamhuri ya Afrika ya Kusini kwa ajili ya hatua zinazofuata za mchakato wa usajili na uthibitishwaji. Usafirishaji utafanyika kwa kuzingatia mahitaji ya Afya ya Mimea yaliyowekwa na nchi ya Afrika ya Kusini pamoja na taratibu nyingine zinazotumika.

## 5. MUHIMU KWA WAOMBAJI

TPHPA inawasisitiza Wafanyabiashara, Wakulima, na Wadau wenye nia ya kusafirisha Parachichi na Ndizi Mbichi kwenda Afrika ya Kusini kuwasilisha maombi na nyaraka kamili mapema kabla ya tarehe **06 Oktoba 2026.**

Kuchelewa kuwasilisha maombi au kutokamilika kwa nyaraka zinazohitajika kunaweza kusababisha mwombaji kutofanyiwa ukaguzi kwa wakati na hivyo kutojumuishwa katika mchakato wa uwasilishaji wa taarifa kwa NPPO ya Afrika ya Kusini kwa hatua zaidi.

Wadau wote wanahimizwa kuzingatia matakwa ya Afya ya Mimea katika hatua zote za uzalishaji, ufungashaji, uhifadhi na usafirishaji ili kuwezesha biashara salama ya bidhaa za mimea na kulinda afya ya mimea katika nchi zote mbili.

## 6. UWASILISHAJI WA OMBI

Maombi yawasilishwe kupitia barua pepe: dg@tphpa.go.tz au kwa simu: +255 782 146 161.

Imetolewa na

Prof. Joseph C. Ndunguru

**MKURUGENZI MKUU**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA (TPHPA)**

**"TPHPA AFYA YA MIMEA, AFYA YA MIMEA TPHPA"**